Jibu: Tusome,

“Ganjo” ni mahali palipoharibika.. Jengo lililoharibika linaitwa “Ganjo” yakiwa mengi yanaitwa “maganjo”, mji ulioharibiwa aidha kwa vita au kwa janga fulani pia unaitwa “Ganjo”.

Katika biblia neno hili limeonekana mara kadhaa..

> *Walawi 26:30 “Nami nitapaharibu mahali penu palipoinuka, na kuziangusha sanamu zenu za jua, nami nitaitupa mizoga yenu juu ya mizoga ya sanamu zenu; na roho yangu itawachukia.*
>
> *31 Nami nitaifanya MIJI YENU IWE MAGANJO, na mahali penu patakatifu nitapatia ukiwa; wala sitasikia harufu ya manukato yenu yapendezayo.*
>
> *32 Nami nitaitia hiyo nchi ukiwa; na adui zenu watakaokaa huko wataistaajabia”*

Tusome pia…

> *Ezekieli 29:12 “Nami nitaifanya nchi ya Misri kuwa ukiwa, kati ya nchi zilizo ukiwa, na miji yake, kati ya miji iliyoharibika, ITAKUWA MAGANJO muda wa miaka arobaini; nami nitawatawanya Wamisri kati ya mataifa, nami nitawatapanya kati ya nchi mbalimbali.”*

Neno hili pia unaweza kulisoma katika mistari ifuatayo likiwa na maana hiyo hiyo..*Walawi 26:33, 2Nyakati 34:6, Ayubu 3:14, Isaya 6:11, 7:19, Yeremia 4:7, Ezekieli 6:14, 36:38, na Amosi 9:14.*

Vile vile hii dunia siku moja itafanyika kuwa “GANJO”, kutokana na dhambi!.. Bwana ataiharibu kwa moto kama alivyoiharibu nyakati za Nuhu, kwa maji.

> *2Petro 3:6 “kwa hayo dunia ile ya wakati ule iligharikishwa na maji, ikaangamia.*
>
> *7 Lakini mbingu za sasa na nchi zimewekwa akiba kwa moto, kwa neno lilo hilo, zikilindwa hata siku ya hukumu, na ya kuangamia kwao wanadamu wasiomcha Mungu”.*

Je umeokoka? Kama bado, saa ya wokovu ni sasa, tupo mwisho wa nyakati.

Maran atha.

Tafadhali shea na wengine ujumbe huu;

Pia Kwa maombezi/ Ushauri/ Maswali/ Whatsapp:
Tuandikie katika BOXI la Maoni hapo chini au
Piga namba hizi: +255789001312 au +255693036618

Mada Nyinginezo:

Agano ni nini? na kuna aina ngapi za maagano?[1]

Miji ya Tiro na Sidoni ni miji gani kwasasa?[2]

Kama Malkia Esta alijipamba je! Kuna ubaya gani wanawake wa wakikristo wa leo kujipamba?.[3]

TAA YA MWILI NI JICHO,[4]

VICHEKESHO NA UTANI MADHABAHUNI[5]

Rudi nyumbani[6]

Share on:
WhatsApp
Endnotes:

1. Agano ni nini? na kuna aina ngapi za maagano?: https://wingulamashahidi.org/2022/08/15/agano-ni-nini-na-kuna-aina-ngapi-za-maagano/
2. Miji ya Tiro na Sidoni ni miji gani kwasasa?: https://wingulamashahidi.org/2022/11/29/miji-ya-tiro-na-sidoni-ni-miji-gani-kwasasa/
3. Kama Malkia Esta alijipamba je! Kuna ubaya gani wanawake wa wakikristo wa leo kujipamba?.: https://wingulamashahidi.org/2021/05/18/kama-malkia-esta-alijipamba-je-kuna-ubaya-gani-wanawake-wa-wakikristo-wa-leo-kujipamba/
4. TAA YA MWILI NI JICHO,: https://wingulamashahidi.org/2023/07/09/taa-ya-mwili-ni-jicho/
5. VICHEKESHO NA UTANI MADHABAHUNI: https://wingulamashahidi.org/2020/02/02/vichekesho-na-utani-madhabahuni/
6. Rudi nyumbani: https://wingulamashahidi.org